

# **Mtindo katika Hotuba za Rais J.P. Magufuli na Mchango wake katika Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili**

Ahmad Y. Sovu

## **Ikisiri**

Baada ya Mheshimiwa J.P. Magufuli kutawazwa kuwa Rais wa Tanzania, shughuli zake rasmi za kila siku zilihusisha matumizi ya Kiswahili. Makala yanaeleza: (i) Vibainishi vya mitindo ya lugha ya kisiasa anavyovitumia katika hotuba zake (ii) Ikiwa matumizi ya lugha katika hotuba yana mchango katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Makala yanadhihirisha kuwa katika hotuba hizo Rais Magufuli hutumia vibainishi vifuatavyo: istilahi maalumu, nafsi ya kwanza wingi na umoja, misemo, uradidi wa maneno, lugha ya matumaini, takwimu, balagha, mzaha, lugha yenye mshikamano na lafudhi za lugha za makabila. Makala inabaini mchango wake katika maendeleo ya Kiswahili kuwa ni: Kukuza fasihi ya Kiswahili, kukuza msamiati wa Kiswahili, kuongeza fursa za ajira kwa wataalamu wa Kiswahili, kuwatia ari wakalimani, wafasiri na pia kuwahimiza wananchi katika kuthamini matumizi ya lugha ya Kiswahili. Makala inatoa mchango mkubwa katika uga wa lugha ya siasa kwa kudhihirisha namna vipengele anuwai vya lugha ya kisiasa vinavyotumika katika hotuba za viongozi wa kisiasa na taathira yake katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

## **1.0 Utangulizi**

Matumizi ya lugha ni namna ambavyo wazungumzaji wa lugha huitumia lugha kwa kuzingatia mila, desturi na kaida mbalimbali za jamii katika muktadha husika. Kwa kiasi kikubwa matumizi hayo ya lugha hutegemea muktadha (Masebo na Nyangwine, 2004). Aidha, wanasiasa nao hutumia lugha kulingana na muktadha wao, yaani eneo la mkutano au shughuli yoyote ile ya kijamii wanayoifanya.

Matumizi ya lugha katika muktadha wa kisiasa kama dhana, hufafanuliwa kwa namna ambavyo wanasiasa huitumia lugha kufikisha ujumbe waliokusudia kwa jamii. Kwa kawaida, lugha ya wanasiasa hutofautiana na lugha ya kawaida (Joseph, 2006); wanasiasa hutumia vipengele fulani vya lugha kufikisha ujumbe wao kwa jamii. Makala haya yamekitwa katika kushughulikia suala la lugha kama lilivyojitokeza katika hotuba za Rais J.P. Magufuli na kudhihirisha mchango wake katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Kupitia hotuba zake kadhaa, tumechunguza mitindo ya lugha ambayo huitumia katika kutoa ujumbe mbalimbali kwa Watanzania na jamii ya kimataifa.

Katika makala haya, tumejaribu kuonesha jinsi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. J.P. Magufuli, anavyotumia vibainishi mbalimbali vya lugha katika hotuba zake kwa hadhira anuwai anapozihutubia. Pia, makala inafafanua mchango wake katika fani za lugha kama vile fasihi, kukuza msamiati wa Kiswahili na kuonesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili na namna Tanzania inavyoweza kupiga hatua za maendeleo ya Kiswahili kupitia Magufuli.

Data za makala haya, zinatokana na usikilizaji wa hotuba hizo za kipindi cha baina ya mwaka 2016 hadi 2018 kutoka katika mtandao wa kuhifadhi video wa “youtube” na kisha kuzinukuu katika maandishi. Kabla ya kuanza kudavua kwa kina juu ya mchango wa Rais Magufuli katika lugha ya Kiswahili, ni vema kueleza historia yake kwa ufupi.

### **1.1 Historia Fupi ya Rais Magufuli na Tajiriba yake Kisiasa**

John Pombe Joseph Magufuli alizaliwa tarehe 29 Oktoba, 1959 wilayani Chato, mkoa wa Kagera (sasa mkoa mpya wa Geita). Ndiye Rais wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alichaguliwa Oktoba 2015 na kurithi mikoba ya Jakaya Mrisho Kikwete. Magufuli ni mwanasiasa mwenye sifa ya uchapakazi na asiye na mzaha. Magufuli au JPM kama anavyofahamika, alichaguliwa kwa mara ya kwanza 1995 katika nafasi ya ubunge, na akadumu katika baraza la mawaziri katika nafasi ya Naibu Waziri wa Ujenzi kuanzia 1995 hadi 2000, Waziri wa Ujenzi kuanzia 2000 hadi 2006, Waziri wa Ardhí na Maendeleo ya Makazi mwaka 2006 hadi 2008, na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Samaki 2008 hadi 2010, Waziri wa Ujenzi kwa mara ya pili kuanzia 2010 hadi 2015. Alisimama akiwa mgombea wa nafasi ya urais kupitia chama tawala-Chama cha Mapinduzi CCM, akashinda uchaguzi wa 2015 na kuapishwa Novemba 5, 2015. Rais Magufuli kitaaluma ni mwalimu na mtaalamu wa kemia na hisabati. Ana digrii ya uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **Dhana ya Mtindo na Mkabala wa Kinadharia**

### **2.1 Dhana ya Mtindo**

Mwansoko (1991) anasema mitindo ni dhana inayowakilishwa na neno “mtindo” haikujitokeza wala kujengeka ghafla tu. Dhana hii ina historia ndefu. Hapo zama za kale Wagiriki na Warumi waliuelewa mtindo kuwa ni balagha (*rhetory*), yaani utaalumu wa kutumia maneno mengi na yaliyo mazuri lakini yasiyo na maudhui makubwa. Mtindo ulichukuliwa kuwa ndio nyenzo au mbinu za kushawishi wasikilizaji wavutiwe, wasadiki na wayakubali yasemwayo na mzungumzaji. Mwansoko (keshatajwa) anafafanua kuwa mtindo ni tabia ya upekee za uzungumzaji wa kila mtu, kila mwanajamii. Anahitimisha

kwa kusema kwamba licha ya kuwa ni upekee wa mzungumzaji, lakini mitindo ni mifumo ya zana za kiisimu inayoambatana na kazi au shughuli moja maalumu ya jamii, kama vile, shughuli za kijamii na kisiasa, shughuli za kisheria na utawala na kadhalika. Naye Okwena (2017) akiwanukuu (Buffon 1930; Crystal na Davy 1969) wanasema mtindo ni mtu mwenyewe yaani, jinsi mtu anavyotumia lugha kupitisha ujumbe wake. Kwa ujumla, tunaweza kusema mtindo ni namna mwandishi au msemaji anavyoamua kuteua vipengele fulani vya lugha ili aweze kufikisha ujumbe wake kwa hadhira katika hali ya kueleweka na kwa wepesi.

## **2.2 Mkabala wa Kinadharia**

Makala haya yamejadiliwa kwa kuzingatia Nadharia ya Elimu-mitindo iliyoanzishwa na kutumiwa na Jakobson (1960) na Murry (1976). Jilala, (2016: 127), anaeleza kuwa Elimu-mitindo ni taaluma inayoshughulikia mtindo. Ni taaluma ya mitindo mbalimbali ambayo inajitokeza katika mazungumzo, ama maongezi fulani au maandishi ya matini fulani. Ujitokezaji wa ufanano wa aina fulani wa muundo, dhana ya kizungumzwa, kitamkwa, ama matini ni mambo yanayoshughulikiwa na elimu-mitindo. Mwansoko (1991: 4-5) kwa upande wake anafafanua kuwa, elimu-mitindo ni taaluma inayohusiana na vipengele vyote vya muundo wa lugha. Yaani ni taaluma inayochunguza misingi na matokeo ya uchaguzi na matumizi ya maneno, sarufi yake, mofolojia na aina nyingine za vipengele vya lugha kama mbinu za uhamishaji mawazo na hisia za mwandishi au msemaji katika mazigira ya mawasiliano. Mwansoko (keshatajwa) akihitimisha kuhusiana na nadharia hii ya elimu-mitindo anasema, elimu-mitindo inahusiana na vipengele vyote vya lugha. Uchunguzi wa elimu-mitindo, na hasa umuhimu wa mitindo unaambatana sana na matumizi ya lugha katika mawasiliano, yaani utendaji kazi wa lugha. Maelezo haya ya Mwansoko tumeyapa umuhimu mkubwa na kuamua kutumia Nadharia ya Elimu-mitindo ambayo inasisitiza kuwa lugha ina uwezo mkubwa wa kuibua miguso mbalimbali na utendaji kazi katika mazingira yanayotofautiana. Kwa sababu elimu mitindo inachagua vipengele mbalimbali vya kiisimu (mitindo) ili vitumike kutokana na mazingira, mada, kusudi na njia ya utekelezaji wa mawasiliano. Kwa hivyo, tumetumia Nadharia ya Elimu-mitindo katika uchambuzi wa hotuba za Rais Magufuli katika kuchunguza mitindo anuwai ya lugha ya kisiasa kama vile uradidi, misemo, tashtiti, takwimu na kadhalika, kwa lengo la kuchunguza ni jinsi gani mitindo hii hutumika katika kuipamba na kuirembesha lugha yake lakini pia, ni kwa namna gani inachangia kuleta maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

## **2.0 Mtindo wa Lugha ya Kisiasa katika Hotuba zake**

Katika kuchambua vipengele vya kisiasa, kuna ajenda mbalimbali huzingatiwa. Miongoni mwa ajenda hizo ni vipindi vya kihistoria kama siasa za Ujamaa na Kujitegemea, Azimio la Arusha, Uchaguzi Mkuu n.k. Katika makala haya, kwa kuzingatia usikilizaji wa hotuba za Magufuli zilizohifadhiwa katika mtandao wa “youtube” na kupitia tovuti ya [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz) tumeonesha vibainishi au mitindo mbalimbali ya lugha anayoitumia katika mikutano yake mbalimbali kama ifuatavyo:

### **3.1 Matumizi ya Istilahi na Msamiati Maalumu**

Wanasiasa hutumia msamiati au istilahi zinazowakilisha dhana fulani katika kampeni maalumu (Mills, 1984). Hali kama hiyo ya kutumia msamiati maalumu imejitokeza katika hotuba za Rais Magufuli. Tuchunguze mfano wa 1 katika dondoo lifuatalo:

*...wajenge viwanda hapa hapa na bahati nzuri wanaposafirisha ile wanakwambia **Titaniumu, Copper au Zink. Process** yake ni ndogo mno wanatumia kitu kinaitwa “**boiling point**” wajenge **furnance** zao hapa, vijana wetu wapate ajira hapa, wasafishe hapa madini, tutajua **Tatinium** kiasi gani? **Zink** kiasi gani? **Lead** ni kiasi gani? **Copper** ni kiasi gani? Tanzania tupate fedha...tumechezewa vya kutosha...*

(Hotuba ya Magufuli kwa Wachimba Madini Shinyanga, 6 Septemba, 2016)

Katika dondoo hapo juu tunabaini kuwa, Magufuli ametumia msamiati au istilahi mahususi zinazoendana na muhtadha wa masuala yanayohusu madini. Kwa mfano, Magufuli ametumia maneno kama vile **titanium**, (*aina ya madini ya titanium*) **Copper** (*shaba*), **Zink** (*zinki*), **process** (*mchakato*), **boiling point** (*kiwango cha jotoridi*) na **Lead** (*risasi, aina ya metali*) **furnance** (*tanuru la kuchemsha joto kubwa zaidi ya 700 sentigredi*); maneno yote yanaashiria kuwa masuala hayo yanahusiana na madini, hasa ukizingatia muhtadha aliokuwa akiuhutubia ni wa wachimbaji wa madini na watu mbalimbali wanaojua masuala ya madini. Uteuzi wa msamiati maalumu unaoshabihiana na muhtadha unaonesha umakini wake, unasaidia kuvuta hisia za wananchi na humwona kiongozi husika kuwa anajua vyema masuala yanayowakabili.

### **3.2 Matumizi ya Nafsi ya Kwanza Umoja na Wingi**

Aidha, wanasiasa hutumia vipengele vya lugha kwa malengo maalumu. Wakati mwingine hutumia nafsi ya kwanza wingi kwa hadhira ileile (Brown na Gilman, 1960). Magufuli naye hutumia nafsi mbalimbali ikiwamo nafsi ya kwanza umoja na wingi katika hotuba zake. Tuchunguze mfano katika dondoo lifuatalo:

- (2) ...*Ninawaambia ndugu zangu, Mimi nimekaa serikalini miaka 20, hao wanaopiga kelele wengine hao mnaowasikia sijui walikuwa wapi? Mimi miaka 20 nikiwa Waziri, nikiwa Mbunge, Tanzania ninaifahamu, lakini leo jamani mimi ndio Rais, hakuna mtu anayejua siri za serikali kama Rais...*

(Mkutano wa Ufunguzi wa Barabara ya Manyoni-Itigi-Singida, 25 Julai, 2017)

Katika dondoo hapo juu tunaona kuwa Magufuli ametumia nafsi ya kwanza umoja, ‘**ninawambia, mimi, nimeka, nikiwa, ninaifahamu**’. Makala haya yamebaini kuwa kwa kutumia nafsi ya kwanza ya umoja na wingi, anaonesha kwamba yeye mwenyewe (binafsi) anaijua nchi vizuri. Kwa hivyo, hataki raia wadanganywe na kusikiliza maneno kutoka kwa watu wengine, kwani itakuwa uzushi na uongo badala yake wamsikilize yeye tu.

### 3.3 Ubadilishaji Msimbo

Kwa mujibu wa (Sylvester, 2011), ubadilishaji msimbo ni hali ya utumizi wa lugha mbili au zaidi katika tamko moja, au mfuatano wa matamko kati ya wazungumzaji wawili au zaidi. Hali hiyo inayofafanuliwa na Sylvester (keshatajwa), wakati mwingine hutumiwa na Magufuli katika hotuba zake; Magufuli hutumia Kiingereza na Kiswahili hasa anapozungumza na hadhira yenye uelewa wa lugha hiyo. Makala haya yamebaini kuwa, Rais Magufuli hutumia zaidi lugha ya Kiingereza hasa pale anapotaka kuonesha hisia zake za ndani, na kutia msisitizo wa jambo analolikusudia kwa wananchi. Tuangalie mfano wa 3 ufuatao:

- (3) ...*Unapooona watu wanashangaa shangaa sana, kwa sababu hawakuzoea haya, na walifikiri nitakuwa **part of them, never...** (Makofi) **not me**, ni mara kumi nisiwe Rais nikachunge hata nini, nikakae kijijini huko kuliko kuwa Rais na nivumilie uozo huu unaofanyika, **I'm saying never**. Nitawashughulikia kwelikweli!.. watu lazima wabadilike, lazima tubadilike, **that is my direction and I will never change it...***

(Ufunguzi wa Mkutano wa Bodi ya Usajili ya Makandarasi - Dar es Salaam, 26 Mei, 2016)

Katika dondoo la hapo juu, tunabaini kuwa kuna matumizi ya maneno ya lugha ya Kiingereza yaliyotumika pamoja na ya lugha ya Kiswahili, maneno hayo ni *part of them* (sehemu ya mafisadi), *never* (kamwe haiwezekani), *not me* (Labda nisiwe mimi Magufuli) *I'm saying never* (ninasema kamwe haiwezekani) *that is my direction and I will never change it* (huo ndio mwelekeo wangu na sitoubadilisha). Matumizi ya kubadili msimbo katika Kiswahili na Kiingereza,

kwa maoni yetu yametumiwa na Magufuli kwa lengo la kuonesha msisitizo kuwa yeye sio Rais wa kufanyiwa mzaha mzaha, na hataki mambo ya ufisadi.

### **3.4 Matumizi ya Misemo**

Mwangi na Munyao (2016: 129), wanasema misemo ni maneno yanayotumiwa kuleta maana tofauti na maana halisi ya maneno yanayotumika. Kwa mfano, msemu *kula chumvi nyingi* haumaanishi kula chumvi halisi bali unamaanisha kuzeeka. Mwangi na Munyao (weshatajwa) wanaendelea kufafanua kuwa, misemo ni kipera cha tungo fupi katika fasihi simulizi na hutumiwa sana kama tamathali ya lugha. Wakimnukuu Senkoro (1982) wanasema kuwa, misemo hutumika mara kwa mara katika mazingira maalumu kuleta maana maalumu. Misemo hutumiwa kutoa ujumbe kwa muhtsari, kuficha maneno makali kwa kutumia maneno mengine, kuhifadhi amali za jamii na pia kupamba lugha. Magufuli, ametumia misemo katika mazingira maalumu na shabaha maalumu kama ifuatavyo:

- (4) *...ni kweli bomba hili lingeweza kwenda mahali popote, na siku zote mwamba ngoma huvutia kwake, na mimi niliivuta kweli ngoma kweli pamoja na wataalamu wa Tanzania...*

(Mkutano wa Uwekaji wa Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi-Chongoleani-Tanga, 05 Agosti, 2017)

Katika mfano huu tunabaini kuwa, Mheshimiwa Magufuli ametumia msemu *'mwamba ngoma huvutia kwake;'* msemu huu una maana kuwa, katika ushindani wa suala lolote basi kila mmoja huvutia upande wake. Msemu huu unaonesha uhalisia kuwa, suala la Tanzania kupata nafasi ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania huenda halikuwa jambo jepesi sana, na pengine kulikuwa na ushindani na nchi nyingine ndio maana akatumia msemu kila mwamba ngoma huvutia upande wake, akimaanisha kuwa yeyé na wataalamu wake walitoa hoja nzito za kuvutia upande wao.

### **3.5 Takriri/Uradidi wa Maneno**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 302), uradidi ni istilahi inayotumiwa kuelezea sifa ya kurudiwarudiwa kwa neno au sehemu ya neno. Katika hotuba za Magufuli tumebaini kuwa hutumia kibainishi cha uradidi katika hotuba zake mbalimbali anapokuwa akiwahutubia wananchi wake. Tuangalie mfano ufuatao hapa chini:

- (5) *...Kwamba tumepewa nchi hii na Mwenyezi Mungu, Mungu hakukosea, makabila yote 121 kuyaweka Tanzania alikuwa na makusudi yake, Mungu hakukosea kuziweka dhahabu hapa Tanzania hakupeleka nchi nyingine,*

*Mungu hakukosea kutuwekea Tanzanite Tanzania, madini yanayopatikana Tanzania tu...*

(Ufunguzi wa Barabara ya Manyoni-Itigi-Singida, 25 Julai, 2017)

Katika mfano huo tunamaizi namna Magufuli alivyolirudia maneno ‘*Mungu hakukosea*’. Lengo la kurudia ni kuonesha msisitizo kuwa rasilimali za nchi zinazopatikana Tanzania zimeletwa kwa mapenzi ya Mungu mwenyewe.

### **3.6 Lugha yenye Kutoa Matumaini**

Moja ya matarajio ya wananchi kutoka kwa viongozi wao, ni kusikia mambo mazuri au mipango mizuri itakayoleta faraja kwao. Magufuli kama ilivyo kwa viongozi wengine, naye hutumia lugha yenye mwelekeo wa kutoa matumaini kwa wananchi wake. Lugha hiyo kwa maoni ya makala haya huwa imetawaliwa na nasaha na ushauri kwa wananchi. Tuangalie mfano ufuatao:

- (6) *...Lakini niwaombe pia wananchi, mtoe ushirikiano mkubwa kwa Waheshimiwa madiwani, madiwani wanawawakilisha ninyi, mtoe ushirikiano mkubwa kwa Mheshimiwa mbunge Koka, anajitahidi kufanya kazi, hatukuchagua malaika, lakini anajitahidi. Kuongoza ni msalaba! Naomba mtoe ushirikiano mkubwa, naomba mtoe ushirikiano mkubwa kwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Watendaji na Wafanyakazi wote katika maeneno mbalimbali, najua changamoto bado ziko nyingi, hatuwezi tukazimaliza siku moja: kuna changamoto za ardhi, kuna changamoto za viwanja...*

(Mkutano katika Ziara yake na Wananchi-Kibaha-Pwani, 20 Juni, 2017)

Katika mfano hapo juu, tumebaini matumizi ya lugha yanayotoa matumaini, na kuhimiza ushirikiano kwa jamii pale anaposema; *najua changamoto bado ziko, hatuwezi kuzimaliza siku moja*, lakini pia anahimiza ushirikiano pale anapowataka wananchi watoe ushirikiano kwa viongozi wao na watendaji wa serikali.

### **3.7 Matumizi ya Lugha yenye Takwimu**

Makala haya yamebaini pia, Magufuli hutumia lugha yenye takwimu katika hotuba zake. Lugha ya takwimu ni matumizi ya lugha yenye data zinazoelezea na kufafanua masuala mbalimbali kwa mahesabu. Katika hotuba zake, wakati mwingine hutumia takwimu ili kuongeza nguvu ya ushawishi wa hoja zake anazoziwasilisha kwa wananchi. Tuangalie mfano ufuatao:

- (7) *...Ndege zile za jeti, unapotoka hapa kwenda Mwanza kwanza utatumia mafuta mengi, ukitumia ndege ya jeti kutoka hapa mpaka Songea, utatumia milioni Ishirini na nane za kununua mafuta point tisa,*

*ukitumia ndege hii ni shilingi milioni moja (makofi) kwa hiyo kwa watu wanaofanya biashara lazima waipige vita, na utofauti wa kufika ni dakika ishirini, dakika ishirini ukichelewa wewe zinakuuma nini? Na ndio maana yule aliyezungumza anataka spidi nikamwambia kapande za jeshi (kicheko/makofi) ili akafike haraka anakotaka. Tunafanya biashara na biashara lazima uangalie mazingira yote...*

(Uzinduzi wa Ndege Mbili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa-Dar es Salam, 28 Septemba, 2016)

Magufuli ametumia takwimu hizo za mahesabu kuonesha tofauti ya kiwango cha mafuta kinachotumiwa na ndege hizo. Matumizi ya takwimu hizo yalikuwa yanalenga kushawishi wananchi kuthamini ndege hizo na kuonesha bayana kuwa hazina matumizi makubwa ya mafuta, lakini pia kujibu hoja za watu waliodai kuwa ndege hizo ati hazina spidi.

### **3.8 Matumizi ya Balagha na Mzaha**

Balagha kwa mujibu wa Mogambi (2005), ni maswali ya kawaida ambayo hayahitaji majibu. Nia yake ni kuwazindua wasomaji au wasikilizaji ili wazingatie na kuyafikiria yanayorejelewa zaidi. Maswali ya balagha hukusudia kuleta uchochezi akilini mwa msomaji au msikilizaji ili avute tafakuri fulani. Mbinu hii imetumika katika hotuba zake Magufuli kama ifuatavyo:

- (8) *...Niwaombe Watanzania tusipuuze vitu vyetu, hata kama hukitaki, basi si nafuu ukae kimya, kiherehere cha nini? Tumezoea kusifia watu wengine, kwa nini tusijisifie sisi? (makofi). Hii ndege wala haikuandikwa CCM (kicheko.) Kwa hiyo Mstahiki Meya atapanda, Mbowe atapanda, Lipumba atapanda, CCM atapanda, asiye na chama atapanda, hata mwenye hirizi zake atakaa nazo mfukoni atapanda kwenye ndege hiyo (kicheko), ni ndege ya Watanzania, ni lazima tujifunze sisi Watanzania kujivunia Utanzania wetu.*  
(Uzinduzi wa Ndege Mbili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa-Dar es Salam, 28 Septemba, 2016)

Tunaona katika mfano huu, Magufuli anajaribu kuikumbusha jamii juu ya umuhimu wa kupenda na kuthamini vitu vyao. Matumizi ya maswali ya balagha *Kiherehere cha nini? Kwa nini tusijifie sisi?* – yanajenga fikra pevu ya kuthamini vya kwetu. Pia, kuna matumizi ya lugha ya mzaha au utani fulani kama alivyosema *hata wenye hirizi watapanda*. Kwa maana ndege hizo zina faida kwa Watanzania wote.

### **3.9 Lugha ya Mshikamano**



Makala haya yamebaini kuwa katika hotuba zake mbalimbali, Magufuli hutumia lugha yenye kuonesha mshikamano na umoja wa taifa lake. Tazama mfano wa (9) katika dondoo hapa chini:

(9) ...Ndugu zangu wana Mwanza, nashukuru sana tumefika salama,.. Nataka Watanzania wa maisha ya juu, maisha ya katikati na wa maisha ya chini wote ni Watanzania...(Makofi) nataka kuwahakikishia, na ninamuomba sana Mwenyezi Mungu, nifanye kazi kwa ajili ya watu na hasa watu wanyonge, ninachowaomba ndugu zangu tuendeleo kushirikiana, tuwe pamoja, tumtangulize Mungu, tusibaguane, sisi wote lengo letu liwe ni moja, kuleta maendeleo ya Watanzania wote...(makofi).

(Mkutano na Wananchi Viwanja vya Furahisha-Mwanza, 2 Agosti, 2016)

Katika dondoo hapo juu inadhihirisha kwamba, Magufuli hutumia lugha yenye kuonesha mshikamano na umoja wa kitaifa hususani pale anaposema *tuwe pamoja, tumtangulize Mungu, tusibaguane, sisi wote lengo letu liwe ni moja...*

### **3.10 Matumizi ya Lafudhi kulingana na Muktradha**

Aghalabu Magufuli hutumia lafudhi na/au lugha za jamii zinazoendana na muktradha anaouhutubia. Kulingana na *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (BAKITA, 2015:534) lafudhi au lafidhi ni ubainisahaji wa mtu au jamii ya watu katika utamkaji wa maneno ya lugha wanayoitumia. Matumizi ya lafudhi za baadhi ya lugha za jamii hutumiwa na Magufuli katika mikutano mbalimbali. Tazama mfano wa 10 katika dondoo hapa chini:

(10) *Kasulu hoyeee-(Hoyeee)- Mwiriwe! Nakavubu! Mrakomeye (Turakomeye), na nyie ndakomeye!!...* (Makofi na kicheko)

(Ziara ya Rais Magufuli Kasulu-Kigoma, 22 Julai, 2017)

Kulingana na dondoo hapo juu, utafiti huu umebaini kuwa, matumizi ya lafudhi ya lugha za makabila<sup>1</sup> yana shabaha ya kuonesha kuwa, Magufuli akiwa ni kiongozi wa nchi basi kwanza ana ufahamu wa lugha mbalimbali za makabila. Lakini pia anaonesha kuwa yeye ni sehemu ya kila jamii na yuko pamoja nao.

### **4.0 Mchango wake katika Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili**

Sehemu hii inabainisha mchango wake katika kuleta maendeleo ya Kiswahili. Haya tumeyabaini kupitia hotuba zake mbalimbali azitoazo katika mikutano

---

<sup>1</sup> Lugha za makabila ni lugha inayozungumzwa na wenyeji wa eneo fulani au kabila fulani

tofautitofauti wakati wa utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku, na matamko yake yanayoonesha msimamo wake kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli anuwai za serikali, kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo:

#### **4.1 Matumizi ya Kiswahili katika Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa**

Miaka ya nyuma wataalamu mbalimbali na wanahakarati wa Kiswahili walikuwa wakilalamika kuhusiana na msukumo wa matumizi ya Kiswahili kwa viongozi wetu wa kisiasa. Kwa mfano, Mulokozi, (2005:15) anaeleza:

Kwa bahati mbaya, msukumo huo wa kisiasa haupo tena. Serikali (kwa maana ya viongozi wakuu wa serikali, mbali na uongozi wetu wa “utamaduni” ambao ndio kazi yao), haisimamii tena kwa karibu na kuipa msukumo juhudi za kukuza Kiswahili...

Hali kwa sasa ni tofauti kidogo, ambapo Rais Magufuli amekuwa akitumia Kiswahili katika shughuli zake zote za serikali. Hadi hivi karibuni tumeshuhudia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) likimpa kongole kwa hatua hiyo ya uzalendo wake wa kuitumia lugha ya Kiswahili katika mikutano mikubwa na hafla mbalimbali za kitaifa na kimataifa kama taarifa inavyonukuliwa hapa chini;

Akiongea na waandishi wa habari leo jijini Dar es Salaam Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi BAKITA, Prof. Martha Qorro, ameeleza msimamo huo wa Rais Dkt. Magufuli umewasidia Watanzania kupata taarifa moja kwa moja kutoka tukio husika.

“Uamuzi na msimamo wa Rais Magufuli wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mikutano mikubwa ikiwemo mkutano mkuu wa 17 wa viongozi wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umepokelewa kwa furaha kubwa na wananchi na wadau wengi wa Kiswahili ndani na nje ya Tanzania” alisema Prof. Martha.

**Chanzo:** maujanja24newz.blogspot.com (14 Machi, 2016)

Wakati Rais Magufuli akitoa hotuba yake ya kumkaribisha Waziri Mkuu wa India Narendra Modi alisema:

Waziri Mkuu Modi kutoka nchi ya India, ambaye anawakilisha populesheni ya watu wengi, lakini ameamua kuja kututembelea Tanzania; ninasema asante sana, na ninyi mliondhorika hapa asanteni sana (makofi). Kwa sababu hotuba yangu nilikuwa naitafsiri mwenyewe hapa kwa Kiswahili, sasa nimpe huyu aisome kwa Kiingereza kama ilivyoandikwa hapa. Ninawashukuru sana, nilitaka nizungumze Kiswahili kwa ajili ya kupromote Kiswahili chetu

(makofi) Mungu ibariki India, Mungu ibariki Tanzania, asanteni sana (makofi)  
(Ziara ya Waziri Mkuu wa India Narendra Modi Ikulu-Dar es Salaam, 10 Julai, 2016)

Mfano hapo juu unadhihirisha bayana kuwa, Rais Magufuli ametumia lugha ya Kiswahili kwa makusudi maalumu hasa ya kukitangaza Kiswahili katika mkutano huo muhimu unaojumuishia viongozi wa Tanzania na India. Hakutaka kusoma hotuba iliyoandikwa kwa Kiingereza badala yake akaamua kuitafsiri yeyé mwenyewe; huu ni utashi wa kisiasa ulioliliwa kwa muda mrefu.

#### **4.2 Kuiongezea Thamani na Hadhi Taaluma ya Ukalimani na Tafsiri**

Mchango mwingine ni kukuza na kuiongezea hadhi na soko taaluma ya tafsiri na ukalimani katika Kiswahili. Mwansoko na wenzake (2006) wanafasili kuwa tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi lugha nyingine, wakati ukalimani ni uhawilishaji wa mawazo yaliyo katika mazungumzo kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Kuanza kwa Rais Magufuli kutumia lugha ya Kiswahili katika mikutano ya kitaifa na kimataifa kumeongeza chachu ya taaluma hii, kwani sasa wataalamu wengi wanaona kuwa hilo ni jambo linalolipa, na ni fursa ya ajira kwa maendeleo ya Tanzania na jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

#### **4.3 Kupanua Matumizi ya Istilahi za Kiswahili**

Akida (2008) akimnukuu Alidina (1975) anaeleza kwamba, ni muda mrefu toka uhimizaji wa shughuli za ukuzaji na uendelezaji wa istilahi na msamiati uanze. Kulingana na hali hiyo, pengine bila kutarajia Rais Magufuli amekuwa naye akifanya jitihada hizo bila hata kung'amua kuwa anasaidia katika ukuzaji na uendelezaji wa istilahi na msamiati. Tazama mfano wa hapa chini utabaini ukweli wa kauli hii:

“...Jamani mnataka mimi nifanyeje? Mnataka nitumbue **jipu** hapahapa? Wangapi wanataka nitumbue jipu hapahapa? (wotee!!)...  
Kwa hiyo, kuanzia sasa Kabwe nimemsimamisha kazi, nendeni mkamwambie (shangwe na makofi)...  
(Uzinduzi wa Daraja la Nyerere-Kigamboni-Dar es Salaam, 19 Aprili, 2016)

Katika mfano wa hapo juu, kuna matumizi ya maneno **tumbua** na **jipu** ambayo kwa mujibu wa *Kamusi ya Kuu ya Kiswahili* yana maana zifuatazo:

**Tumbua:** toboa mahali palipovimba kama vile, kipele au jipu kwa kuminya au kutumia kitu chenye ncha kali

**Jipu:** Uvimbe unaotunga usaha mwilini wenye maumivu makali na ambao hutibiwa kwa kupasuliwa.

Ukiachilia maana za msingi za maneno hayo kama zilivyofafanuliwa kwenye *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, bado katika mfano wa hapo juu, maana zinazojitokeza ni tofauti kulingana na zilivyotumiwa ambapo neno **tumbua** lina maana ya achisha mtu kazi; hali ya kuwa **jipu** inarejelea mtu ambaye yupo katika mazingira ya kazi, lakini wakati wowote ule anaweza kuachishwa kazi kutokana na utendaji usioridhisha. Matumizi ya maneno haya katika muktadha wa matumizi ya kawaida yamekuwa ni jambo la ada kabisa.

Msamiazi mwingine ni matumizi ya neno “**makinikia**.” Neno makinikia limetokana na juhudi za Rais Magufuli, ambaye aliunda kamati iliyoongozwa na Prof. Abdulkarim Mruma kuchunguza viwango vya madini katika makontena yaliyokuwa yakisafirishwa nje ya nchi. Kamati hiyo ilitoa ripoti ambayo ilitumia neno “makinikia” kufasiri neno la Kiingereza “concentrates.” Katika lugha ya Kiswahili neno **makinikia** humaanisha mabaki ya mchanga wa dhahabu baada ya kuchenjuliwa.

#### **4.4 Kuongezeka kwa Misemo Mingine ya Kiswahili**

Misemo ni maneno au kalima ambazo hutumiwa na wanajamii kwa namna maalumu ili kutoa ujumbe maalumu kwa jamii. Rais Magufuli kupitia kaulimbiu na falsafa yake ya kuwataka Watanzania wachape kazi kwa bidii zote, na pia dira yake ya kuifanya nchi ya Tanzania kuwa ya viwanda, ameibua misemo kadha. Baadhi ya misemo hiyo ni:

- (i) *Hapa Kazi tu*
- (ii) *Tanzania ya Viwanda*

Msemo **hapa kazi tu!** umekuwa ukutumika kusesitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii kubwa ili hatimaye nchi ielekee kuwa ya viwanda. Msemo wa *hapa kazi tu* huenda mbali zaidi katika matumizi yake hadi katika masihara ya kawaida; utakuta, mathalani, shuka imetandikwa kitandani na imeandikwa *hapa kazi tuu!* Hii ni kuonesha namna matumizi ya msemo huu yalivyotamalaki katika jamii.

#### **4.5 Kushirikiana na Asasi Zinazokuza Kiswahili**

Rais Magufuli amekuwa akishirikiana na asasi mbalimbali zinazokuza lugha ya Kiswahili, katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya Kiswahili. Mathalani, kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tumemshuhudia Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizindua *Kamusi Kuu ya Kiswahili* iliyotayarishwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) Bungeni – Dodoma, na katika hotuba

yake, pamoja na mambo mengine, alionesha mchango wa Magufuli katika kukuza Kiswahili, kama alivyosema:

Mheshimiwa Mwenyekiti uzinduzi wa kamusi hii unakwenda sambamba na azma ya serikali ya kutumia lugha ya Kiswahili kwenye shughuli zote za kitaifa, kama vile mikutano, mijadala, semina na ufundishaji pia kwenye shule zetu. Azma hii sio ngeni, mataifa mengi duniani yanatumia sana lugha zao kwenye shule zao kwa lengo la kuendeleza na kutangaza pia utamaduni wao. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuanza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mikutano na matukio muhimu ya kitaifa, kama vile dhifa za kitaifa anazowaandalia wageni wake kutoka nje ya nchi, lakini pia na namna ambavyo anakitumia Kiswahili hiki katika nyanja mbalimbali...

(Hotuba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika Uzinduzi wa Kamusi Kuu ya Kiswahili Bungeni-Dodoma, 19 Juni, 2017)

Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa, Rais Magufuli ana ushirikiano na asasi mbalimbali zinazokuza Kiswahili. Isitoshe, mawaziri na watendaji wake wa wizara zake za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wamekuwa wakitoa ushirikiano na asasi mbalimbali za Kiswahili kwa kushiriki katika makongamano, warsha na mikutano ya Kiswahili. Miongoni mwa asasi hizo ni pamoja na: Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA), Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA) na Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili Vyuho Vikuu vya Afrika Mashariki (CHAWAKAMA) kwa kutaja chache tu.

#### **4.6 Kutoa Fursa za Ajira kwa Walimu wa Kiswahili Nje ya Nchi**

Juhudi za Rais za kutumia Kiswahili katika hafla mbalimbali za kitaifa na kimataifa zimefanywa sambamba na juhudi za kupatikana fursa za kufundisha Kiswahili katika nchi mbalimbali zikiwamo Sudan Kusini na Ethiopia, na hivi karibuni Rais ameahidi kupeleka walimu wa Kiswahili katika nchi ya Misri, kama anavyosema:

...Katika mahusiano hayohayo, kwa sasa hivi kuna Watanzania 115 katika masuala ya elimu, ambao wanasoma katika vyuo kule, wameamua kuongeza idadi ya wanafuzi watakaokuwa wanakwenda kusoma Misri, katika sekta ya Elimu na kuwa na *Exchange program*, na kwenye hili nimetoa msukumo kwao, kwamba tutatoa waalimu wa Kiswahili ili waende wakafundishe kwenye vyuo vikuu kule na wao wamekubali pia kutoa waalimu wa IT, wa masomo ya

Sayansi, wa lugha ya Kiarabu na mambo ya dini ili waje kufundisha katika maeneo mbalimbali ya vyuo...

(Hotuba ya Rais Magufuli kwa Rais wa Misri Abdel Fattah El-Sisi Ikulu-Dar es Salaam, 14 Agosti, 2017)

Kulingana na hali hiyo, ni jambo lililo bayana kabisa kuwa Rais Magufuli amechangia ongezeko la fursa za ajira kwa vijana na Watanzania kwa jumla. Kupatikana kwa fursa hizo kutasaidia pia kukieneza na kukiendeleza Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania.

#### **4.8 Kukemea Kasumba**

Mulokozi (2005: 16) anasema kuwa, tatizo la “kasumba” lipo, ingawa siku hizi halizungumzwi. Hili ni tatizo la Mwafrika mweusi duniani kote. Chanzo chake ni kutawaliwa kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi, kidini, kielimu, n.k. Mulokozi (keshatajwa) anasema kuwa hili ni tatizo kubwa kuliko tunavyodhani, na sidhani kama tunafanya juhudi ya kutosha kupambana nalo. Mathalani, katika dunia ya leo ni Mwafrika pekee anayekataa lugha yake, dini yake ya asili, mavazi, teknolojia hata majina ya kabila au taifa lake, na kukimbilia kuiga mambo ya wengine.

Mulokozi anaendelea kufafanua kuwa, Mtanzania mwenye kasumba havezi kukuza Kiswahili, na lazima atapendelea Kiingereza, kwa sababu anaamini kuwa kuongea Kiingereza ndio kuelimika, kuendelea au kustaarabika. Rais Magufuli ni kama aliyemsikia Mulokozi, naye amekuwa na mchango mkubwa wa kukemea na kupambana vikali dhidi ya watu wenye kasumba, ambao wanaamini kujua Kiingereza ndio kusoma na ndio kutaalamika na kuiletea nchi maendeleo. Tazama anavyonena:

...Ninachotaka kusema ni nini? Chalenji kwenye edukesheni ipo. Lakini ni lazima tuwe careful katika kuargue, tusije tukakatili elimu yetu ambayo imeanzishwa na Baba wa Taifa mpaka tumefika hapa, halafu tuanze kujidharau. **Ati mtu amemaliza form four hajui kuandika barua kwa Kiingereza kwani kusoma ni Kingereza? (makofi) Kwani Wachina wanajua Kiingereza? Mbona wanatengeneza silaha za kila aina? Warusi wanajua Kiingereza? Mie nimekaa Ujerumani, Wajerumani hawajui Kiingereza, nimekaa Ufaransa hawazungumzi Kiingereza, ile *shortsighted* inawafanya watu wafikiri Kiingereza ndio lugha. Mie nimesomea Salford University Masters yangu, nilikuwa nazungumza Kingereza, lakini hapa sizungumzi Kiingereza. Masters yangu niliandika kwa Kiingereza...**

(Mkutano wa hadhara na wanajumuiya wa -Chuo cha Elimu Mkwawa, 2 Mei, 2018).

Ukichunguza maelezo ya Rais Magufuli hapo juu, unabaini kwamba naye anakwerwa na baadhi ya watu ambao bado wana kasumba kuwa kujua Kiingereza ndio kusoma. Badala yake anasisitiza na kuwaasa waachane na hizi kasumba kama anavyoendelea kusema:

Kwa hiyo, ninachotaka kuwaambia nyie wasomi wa Mkwawa, na bahati nzuri mnachukua *education*, ninyi muwe kioo cha Watanzania kuwaelimisha. Tanzania tupo kwenye *right truck*, tupo kwenye *direction* nzuri na *IQ* za Watanzania ni kubwa, ninyi ni vipanga (makofi). Imagine umesomea shule za kata mpaka upo chuo kikuu, kwa hiyo, msianze kujiona *weak* au *inferior*, msiwe na *inferiority complex*. Ninyi ni vipanga, na nchi yetu ni ya vipanga na mtaendelea kuwa vipanga...(makofi)

(Mkutano wa hadhara na wanajumuiya wa -Chuo cha Elimu Mkwawa- 2 Mei, 2018)

Kwa hivyo, Hapa tunaona Magufuli anajitahidi kuwajenga moyo vijana, na kuondoa kasumba wajiamini kuwa elimu wanayoisoma ni bora na waithamini.

## 5.0 Matarajio

Kutokana na matamshi au kauli za Rais Magufuli kuhusu maendeleo ya lugha ya Kiswahili, wadau na wananchi kwa ujumla wana matarajio makubwa kwa Rais kuwa, kutokana na msukumo alioanza nao katika kipindi chake cha utawala, baadhi ya vingi vinavyoikabili lugha ya Kiswahili vitatowekaa. Baadhi ya mambo yanayohitaji kushughulikiwa ili kuimarisha lugha ya Kiswahili ni:

- (i) Sera mahususi ya lugha ambayo itabainisha nafasi ya lugha ya Kiswahili, lugha za jamii na lugha za kigeni katika matumizi mbalimbali.
- (ii) Kutumika kwa Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.
- (iii) Kuwa na Ensaiklopedia ya Kiswahili ambayo itaeleza na kufafanua kwa kina maneno dhana na maneno mbalimbali ya Kiswahili.
- (iv) Kuhimiza kupitishwa kwa sheria na kanuni za matumizi ya Kiswahili katika jamii na katika vyombo, shughuli na nyaraka rasmi za kiserikali.
- (v) Kuongeza bajeti kwa asasi za serikali zinazoshughulika na Kiswahili kama vile BAKITA, BAKIZA na vyuo vikuu ili ziweze kuongeza tija na mafanikio katika kukiendeleza Kiswahili.

- (vi) Kuimarisha shughuli za uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na usambazaji wa machapisho hayo ndani na nje ya nchi.
- (vii) Kutumia lugha ya Kiswahili katika kutunga sheria, na kuagiza mahakama zitumie lugha ya Kiswahili, ili wananchi wanyonge, ambao wengi hawaifahamu lugha ya Kiingereza na badala yake wanaijua vema lugha ya Kiswahili, waweze kupata haki na utetezi katika mahakama zao.

## **6.0 Hitimisho**

Katika makala haya tumejadili mtindo wa matumizi ya lugha katika hotuba mbalimbali za Rais Magufuli na mchango wake katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Makala imeonesha vibainishi vya mitindo mbalimbali ya lugha ya kisiasa ambavyo huvitumia katika hotuba zake, kama vile matumizi ya istilahi maalumu, matumizi ya nafsi, uradidi wa maneno, matumizi ya misemo, lugha ya matumaini, matumizi ya balagha na mzaha n.k. Aidha, tumebainisha mchango wake katika kukuza lugha ya Kiswahili kwa kupanua maana ya maneno, kuibua msamiati mpya, kuongeza fursa za ajira za Kiswahili, kukemea juu ya kasumba, kukitumia Kiswahili katika hafla za kitaifa na kimataifa na kuongeza ari kwa viongozi na wananchi wengine kuendelea kuthamini na kuienzi lugha ya Kiswahili. Vilevile, makala imegusia matarajio ya wadau wa Kiswahili na Watanzania wengi kuwa katika zama za utawala wa Magufuli, pengine lugha hii itapiga hatua zaidi kutokana na namna anavyoipa nafasi lugha ya Kiswahili mintarafu umuhimu wake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kiteknolojia na kimshikamano wa kikanda na kitaifa. Kadhalika, makala inatoa mwito kwa viongozi wengine kuanzia wa Tanzania, wa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla, kuendelea kuenzi lugha zetu za Kiafrika na kuzitumia ipasavyo katika kujiletea maendeleo.



## Marejeleo

- Ademilokun, M. (2015). "A Multimodal Discourse Analysis of Some Newspaper Political Campaign Advertisements for Nigerian's 2015 Elections." Lagos: Obafemi Awolowo University.
- Aduradola, R. na Ojukwu, C. (2013). "Language of Political Campaigns and Politics in Nigeria." *Canadian Social Science* 9(3):104-116.
- Akida, H. (2008). "Ukuzaji na Uendelezaji wa Msamiati" katika J.G. Kiango (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. 52-78.
- Crystal, D, & Davy, D, (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group Ltd.
- BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Nairobi: Longhorn Publishers.
- Beard, A. (2000). *The Language of Politics*. London: Routledge.
- Brown, R na Gilman, A.L (1960). "The Pronouns of Power and Solidarity." Katika Thomas A. Sebeok (mh), *Style in Language*, Cambridge, MA: MIT Press, uk. 253-76.
- Chacha, D.S (2006). "Kiswahili and The African States: The Legacy of Mwalimu Julius Kambarage Nyerere" katika *Kiswahili*. Juz ya 69. Dar es Salaam: TUKI. 22-36.
- <http://tubemate.net>
- Jakobson, R. (1987). "Grammatical parallelism and its Russian facet. Language and literature", imehaririwa na Krystyna Pomorska na Stephen Rudy. Cambridge, Mass: Beof Harvard University Press.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, mbinu na matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.
- Joseph, J.E. (2006). *Language and Politics*. Edinburgh: Edinburgh University Press
- Lwaitama A. F (1988). Variations in the Use of Personal Pronouns in the Political Oratory of J.K. Nyerere and A.H. Mwinyi. *Belfast Working Papers in Language and Linguistics* 1, 1-23, Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Masebo, J.A na Nyangwine, N (2004). *Nadharia ya Lugha Kiswahili 1: Kidato cha 5&6*. Dar es Salaam: Afroplus Industries Ltd.
- Maujanja24newz.blogspot.com
- Mogambi, H. (2005). *Mwongozo wa Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Marimba Publishers.
- Mulokozi, M.M (2005). "Baadhi ya Vipingamizi vya Kiutawala vya Kutumia Kiswahili Kufundishia Sekondari na Vyuo" katika *Kioo cha Lugha*. TUKI. 76-81.

- Mwangi, P.K na Munyao, K.J (2016). “Mtindo na Maudhui katika Nyimbo za Kisiasa za Msanii John De’Mathew nchini Kenya” katika *Mulika* TUKI.115-135.
- Mwansoko, H.J.M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mwansoko, H.J.M. (2005). “Mchango wa Mwalimu J.K Nyerere katika Tafsiri na Maendeleo ya Lugha ya lugha,” katika *Kioo cha Lugha*. Kur. 13-21.
- Okwenya, S (2017). “Mtindo wa Jazanda Katika Tamthilia ya Kijiba cha Moyo” katika *Mulika*. TUKI. 58-71.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Sylvester, J. (2011). *Ubadilishaji Msimbo Bungeni na Athari zake kwa Wasikilizaji*, Tasnifu ya M.A Kiswahili (hajachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.  
[www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)  
[www.dw.com](http://www.dw.com) -Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani